



**<u>Agenda ya mwanamme wa kitanzania mwaka 2025</u>**

Ingiwa kuna siku ya Wanaume Duniani, sisi, wanaume wa kitanzania, tunaazimisha **siku ya mwanamme wa kitanzania** kwa mara ya pili tarehe 23 April 2025. Siku ya mwanaume wa kitanzania huazimishwa kila mwaka tarehe 23 Aprili ambayo ni siku chache kabla ya kuazimisha sherehe za muungano wa Tanzania mnamo Tarehe 26 Aprili. Jamhuri ya Muungano wa Tanzania iliundwa mnamo tarehe 26 Aprili 1964. Siku ya mwanaume wa kitanzania ni tofauti na siku ya mwanaume duniani. Na zipo sababu za msingi za kumwazimsha mwanaume wa kitanzania siku tofauti na maazimisho ya mwanaume duniani. Kifupi, mwanzilishi wa siku ya wanaume duniani ni Daktari Jerome Teelucksingh kutoka Trinidad and Tobego ambaye alirasimisha maazimisho hayo siku ya tarehe 19 November 1999. Siku hiyo mwanazuoni huyo aliunganisha tukio hilo na kuazimisha siku ya kuzaliwa baba yake. Hivyo basi, sisi, wanaume wa kitanzania, hatuoni haja ya kusherekea siku ya kuzaliwa ya baba yake Daktari Teelucksingh bali tumeona ni vyema tukio hilo lifanyike siku chache kabla ya kuazimisha siku ya kuzaliwa taifa la Tanzania mnamo tarehe 26 Aprili 1964. Na hiyo ndio sababu ya msingi ya kumwazimisha mwanaume wa kitanzania siku chache kabla ya sherehe za kuazimisha sherehe ya kuzaliwa Tanzania.

Pili, Tanzania imejizolea umaarufu kwa kuwa kisiwa cha amani kinacho thamini ngao zifuatazo: hekima, umoja, na Amani kama inavyo ainishwa katika wimbo wa taifa. Sisi tunamwazimisha mwanaume wa kitanzania kwa sababu yeye ni mtanzania anaye thamini utanzania wake. Hababaishwi na mila na desturi za mataifa ya nje. Yeye anajivunia kuwa mtanzania na ana pigana kulinda nafasi na heshima ya mwanaume wa kitanzania kuanzia ngazi ya familia, jamii, na taifa kwa ujumla.

Katika muktadaha huo, mahusiano mengi ya watanzania wa leo, yamekumbwa na changamoto mbalimbali, ikiwemo mabadiliko ya kijamii na mitazamo ya kijinsia. Wanawake wamehamasishwa kuchukua nafasi za kujitegemea na kushindana katika masuala mbalimbali ya kijamii, hali inayoweza kuathiri matarajio ya kimapokeo katika mahusiano. Kwa upande mwingine, baadhi ya wanaume wanakuwa na wasiwasi kuhusu changamoto za kimaisha zinazoweza kutokea kwenye mahusiano yao, hasa pale ambapo maelewano na heshima ya pande zote hayatimizwi kikamilifu. Ndoa na mahusiano kwa ujumla yanahitaji ushirikiano, maelewano, na kujitolea kutoka kwa wahusika wote ili kufanikisha ushirikiano wa furaha na wa kudumu. Changamoto zinazotokea zinatokana na matarajio ambayo hayalingani, ambapo mahusiano huonekana kama majukumu ya kifedha badala ya ushirikiano wa dhati. Walio

kwenye mahusiano wanapaswa kushirikiana ili kujenga msingi wa heshima ya pamoja na majukumu kwa usawa. Lengo la mahusiano hayo liwe ni kuimarisha mawasiliano, ushirikiano, na heshima ya pande zote ili kuhakikisha furaha na uthabiti katika maisha. Kupitia dhamira ya pamoja na maelewano, changamoto hizi zinaweza kushughulikiwa kwa njia bora.

Watanzania hawana budi kujenga jamii ambapo wake kwa waume na watoto wanaishi kwa hekima, umoja, na amani. Jambo hili siyo rahisi kwa sababu linahitaji uwekezaji katika Nyanja zote na hasa hasa katika kuimarisha mahusiano baina ya wanaume na wanawake. Mazingira ya sasa yana ashiria uwepo wa changamoto katika mahusiano. Inasadikika kuwa kuna ongezeko la idadi ya wanaume wanaotelekezwa na familia zao. Kuna changamoto za mfume dume ambao una nufaisha baadhi ya wanawake na wanaume. Kuna wanawake na wanaume ambao ni wahanga wa unyanyasaji wa kijinsia. Baadhi ya wanaume wanakuwa kama wageni kwenye familia walizozijienga kwa jasho na damu yao. Wanaume hao hujikuta katika mazingira ambapo wenza wao wanawashawishi watoto wao ili wawageuke na kuachwa mwenyewe uzeeni. Lakini pia wapo wanawake wanaoteseka na manyanyaso kutoka kwa wenza wao au ndugu wa wenza zao. Ni ukweli usiopingika kuwa wahanga wako pande zote.

Ingawa changamoto zinazo wakumba wanawake zinasemewa mara kwa mara, changamoto za wanaume hazisemewi vya kutosha. Miradi mingi imejikita kwenye kuwa jengea uwezo wanawake, ikichuliwa kuwa wanaume wote wanauwezo. Baadhi ya wanaume wa kitanzania hawana akiba binafsi za kuwasaidia pindi wanapokuwa wazee na hivyo hujikuta katika hali mbaya baada ya kutekelezwa na familia zao. Baadhi ya wazee wengi walio staafu hujikuta wakianza kutafuta ajira upya ili waweze kujikimu katika maisha yao. Kwa mfano, shirika la SHIWACHANDO (Shirika la Wanaume Wanaopitia Changamoto katika Ndoa) lime baini kuwa migongano mingi katika mahusiano ina husisha wanawake wenye uwezo kiuchumi ambao huwadharau waume zao na kuwa nyima baadhi ya stahiki zao.

Kama walivyoanza wanawake kampeni ya kudai haki zao, wanaume wa kitanzania ni vyema waanzishe kampeni zenye lengo la kuimarisha mahusiano kati ya wanaume na wanawake katika ngazi zote. Malezi ya mtoto yanahitaji uwepo wa baba na mama. Hivyo, anapo kosekana mzazi mmoja wapo, ni tatizo. Ingawa utandawazi na ukuaji wa teknolojia umemwezesha mwanamke kufanya kazi zote ambazo alikuwa akifanya mwanaume, mabadiliko hayo hayatoshi kumsaidia mwanamke katika malezi ya watoto. Mwenendo wa hali ilivyo kwa sasa, unaashiria kuwa utandawazi na ukuaji wa teknolojia, vimeshindwa kusaidia katika malezi ya wototo wa jinsi zote. Na badala yake, vimeleta changamoto kubwa zaidi. Hali imekuwa mbaya zaidi katika mazingira ambapo malezi yanafanywa na mzazi mmoja kulingana na changamoto za utandawazi.

Wanaume walio acha kushika nafasi zao kama wanaume aidha kwa makusudi au kutokana na changamoto katika mahusiano yao, wamesababisha uwepo wa mzigo mkubwa wa malezi kwa wanawake. Kuna kila kiiashiria kuwa mzigo huo, umekuwa mkubwa sana kubebwa. Kwa mfano, imekuwa ni jambo la kawaida kwa mahusiano kuvunjika kwa sababu ambazo siyo za msingi. Lugha gongana hutokea kama utani ambapo amani inatokea dirisha la chumbani na ikirudi

inakaa uvunguni kisha inakuwa ikitambaa kuelekea vyumba vya watoto na kukaa chini ya sofa, nyuma ya luninga ama chini ya meza ya kahawa, yaani ni tafrani tupu.

Wanaume wasiendelee kukaa kimya kwani ukweli usiofichika kuwa utandawazi na teknolojia vimeleta changamoto kubwa zaidi katika mahusiano. Kitendo cha kukaa kimya kwa wanaume kina leta changamoto katika afya ya akili. Changamoto katika afya ya akili huathiri utendaji wa wanaume na wanawake na hivyo kusababisha ukosefu wa tija kwa familia, jamii na taifa kwa ujumla. Pia, udhaifu katika afya ya akili hupelekea matatizo ya magonjwa ya akili. Magonjwa ya akili ni kama magonjwa mengine. Magonjwa hayo yasipo tibiwa hupelekea hali mbaya zaidi ikiwa ni pamoja na vifo kwa wahusika wote.

Kuna maswali ya kujiuliza hapa: je wanaume wa sasa wanaweza kuwalinda wanawake kwa gharama yoyote kuanzia ngazi ya familia, jamii, na taifa kwa ujumla wake kama ilivyokuwa katika jamii zetu za kitanzania hapo zamani? Kwa nini baadhi ya wanawake wanateseka kutokana na kukosa ajira, kuwa wajawazito, na hata kunyonyesha? Kwa nini watoto wa kike na kiume ambao hawa wezi kufanya chochote, wanaendelea kushuhudia chuki, ukosefu wa amani, na njaa.

Mahusiano ikiwa ni pamoja na ndoa yanahitaji ukomavu katika mazingira ambapo wanaume na wanawake wana thamini mahusianao hayo. Wanaume na wanawake wasipo thamini mahusiano baina yao itapelekea uwepo wa changamoto ambazo zitakuwa ni ngumu kutatulika. Katika mazingira yoyote yale, wanawake na wanaume walio kwenye mahusiano wana wajibika kulinda mahusiano hayo na vyote vitokanavyo na mahusiano hayo ikiwa ni pamoja na watoto wao. Na ikitokea changamoto zimepelekea wao kuanzisha mahusiano mengine (al maarufu kama michepuko) kwa kukusudia au kutokana na changamoto zinazo wakumba, wanatakiwa kuwajibika ipasavyo katika nyanja zote ili kuondoa maumivu kwa wahanga na hasa hasa watoto watokanao na mahusiano hayo. Kuwajibika siyo kutoa pesa peke yake bali yawekwe mazingira mazuri ya malezi kwa watoto hao. Haitakiwi, hata kidogo, kuvumilia uwepo wa watoto wa mitaani kwani hiyo siyo mila na desturi ya kitanzania. Uwepo wa watoto wa mitaani unaweza kuleta janga la kitaifa huko mbeleni.

Kwa kuhitimisha, juhudi za kuboresha mahusiano ya kijinsia zinahitaji ushirikiano wa dhati baina ya wadau mbalimbali ikiwa ni pamoja na serikali na wengineo. Pongezi nyingi kwa serikali na wadau wote kwa kutengeneza mazingira wezeshi yaliyo pelekea kufanikisha maazimisho ya siku ya mwanaume wa kitanzania mara mbili mfululizo. Pia pongezi nyingi kwa shirika la SHIWACHANDO (Shirika la Wanaume Wanaopitia Changamoto katika Ndoa) kwa kuendelea kuwasemea wanaume wanaopitia changamoto katika ndoa na kwa mkakati wao wa kuanzisha clinic ya wanaume. Pia tuna wapongeza kwa kuanzisha utaratibu wa kutoa tuzo kwa wanandoa wenye lengo la kujifunza kutoka kwa wanandoa wanaoishi kwa upendo, ustahimilivu, furaha na kutekeleza malengo ya pamoja. Utaratibu huo pia unalengo la kuondoa mitazamo hasi kwa vijana wanaozidi kuchukia ndoa sambamba na kupunguza idadi ya mama au baba anaye lea peke yake (single mothers and single fathers).